MUKHTASARI WA RIPOTI YA UTEKELEZAJI
UTARATIBU WA MASHAURIANO HURU, KABLA YA UANZISHAJI MIRADI

Kuwahamisha watu kutoka kwa maeneo yao ya jadi sio jambo rahisi. Ni lazima pawe na sababu za kutosha kwa hatua kama hii kuchukuliwa. Pia sababu zenyewe zinafaa kukubalika na wenyeji kabla ya kukubali mabadiliko hayo. Wanaosimamia mradi wa kubadilisha maisha ya Jamii - Asili au IP (Indigenous People kwa Kimombo) ni shirika hili la KAPAP lenye mpango wa uzalishaji maliasili, na ukuzaji wa biashara na kilimo nchini.

Mbinu za kufikia malengo na shabaha zake zimeelezwa kwa mukhtasari kwenye makala haya, zikiwa katika sehemu Tatu. (1) Ardhi na maliasili nyingine inayohusika. (2) Ustawishaji wa biashara, utamaduni na maliasili na (3) uhamishaji wa IP kutoka maeneo yao.

Mipango ya kujiandaa kutekeleza mradi wenyewe ni lazima ishugulikiwe kikamilifu na washirika dau wote wahusikao - wakiwa ni pamoja na jamii – husika (IP), Vikao vya wakulima vijijini na wilayani, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA), mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, maafisa wasimamiao utelekelezaji wa miradi, kamati mbali mbali na watoaji huduma, miongoni mwa wengine.

Mikutano hii ya kujiandaa ni lazima iwahusishe waakilishi wa jamii - asili, ili waweze kuelewa manufaa ya kuanzishwa kwa miradi, jinsi itakavyowafaidi kimaisha, kifedha, kimazingira na kuwashirikisha kikamilifu ili kujinufaisha na kukidhi mahitaji yao ya kila siku na hata siku za baadaye. Maoni yao yatakuwa muhimu katika kufikia shabaha na malengo yote ya KAPAP, na ni lazima yaungwe mkono na wenyeji katika maeneo yanayohusika.

Mengineyo yanayozingatiwa ni ukubwa wa eneo, mahali lilipo na hali ya maliasili iliyopo; watumiaji ikiwa ni pamoja na IP na watumiaji kutoka sehemu nyinginezo, jinsi matumizi yote yanavyohitilafiana na madhara – yakiwepo. Mwongozo huru kabla ya kufanywa kwa mashauriano ni muhimu kwa pande zote zinazohusika.

Utaratibu muafaka wa utendaji kazi ni lazima uzingatiwe, hasa inapokumbukwa kwamba uhamishaji wa watu na maisha mapya sio jambo rahisi. Miundo msingi na mikakati ya kuwanufaisha ni lazima itayarishwe kwanza ili kurahisisha shughuli zote za mpango wa KAPAP kote mashinani.

Ufahamu wa matatizo yao ni muhimu; Haya ni pamoja na kunyanyaswa na wanyakuzi wa ardhi, kupoteza haki za kujitambulisha ipasavyo kitamaduni na kijamii, kupokea msaada duni kutoka serikalini, kudunishwa kama jamii na makabila mengineyo, kunyimwa haki zao kisheria ili kufikia maliasili yao na shida za kiuchumi zinazotokana na kuhamishwa kiholela (kutokana na misitu na ardhi waliyotegemea tangu jadi).

Manufaa yanayotarajiwa kwa wote; Ukadiriaji wa watu watakaofaidi, na iwapo faida itagawanywa kisawa kwa wote ni maswala muhimu. Kadhalika, ni muhimu kudadisi na kutambua iwapo miradi inayokusudiwa itawanyima watu (IP) nafasi ya kufikia na kupata ardhi na maliasili yao, iwapo shughuli hizo zitaleta madhara ya uhamisho au kudhuru uchumi, maliasili na mapato yao kwa jumla – na njia za kukabiliana na matatizo hayo yanapojitokeza.

Mengineyo yanayofaa kuzingatiwa ni ; Mbinu za uzimamizi, utunzaji wa maliasili, usimamizi wa ardhi ufaao, kuheshimu haki na tamaduni za watu na kuhifadhi rekodi sahihi za makadirio ya shughuli wakati wote wa kuendesha na kusimamia mipango.

Utoaji wa mafunzo; ili kuhakikisha utekelezaji unaofaa na ukaguzi wa kimazingira na kijamii umefaulu, mpango wa KAPAP utatoa mafunzo ya kimazingira na kijamii yatakuwa muhimu kwa watu wa ngazi tofauti ikiwa ni pamoja na maafisa wa maendeleo ya jamii, vikao vya wakulima vijijini(VFF), DFF, KAPAP – SC na RSU. Makao makuu ya KAPAP pamoja na wataalamu wengineo watatoa mafunzo ya kiufundi.

Mafunzo hayo yatafafanua kwa kirefu jinsi ya kukagua mipango midogo ya jamii, kukadiria maswala ya mazingira na jinsi ya kuyashughulikia. Pia kuna fomu yenye maswala rahisi yatakayosaidia katika utekelezaji wa miradi na utoaji wa ushauri kwa Jamii – Asili (IP). Fomu hizi zitachambuliwa mara nne kwa mwaka kuambatana na mahitaji ya eneo linalohusika.

Habari muhimu kuhusu mradi zitahitajikana zikiwa ni pamoja na jina la wilaya, kikao cha RSU, maafisa wahusika, jina la mradi wenyewe, makisio ya gharama, upana/ukubwa wa ardhi iliyotengwa kwa mradi na shughuli pamoja na mipango mingineyo iliyoshirikishwa.

Maswala ya mazingira; Kuna haja ya kujua mapema iwapo mpango utaleta madhara kama mmomonyeko wa udongo, kuchafua mchanga, kuharibu robuba, kubadilisha mkondo wa maji, kudhuru viumbe wanaoishi majini (samaki), kusababisha upungufu wa mifugo na uzalishaji, kupunguza kiwango cha maji chini ya ardhi au kuleta wanyama wageni na mimea ya kigeni.

Maswala ya kiuchumi na kijamii : itakuwa muhimu kujua iwapo mradi utapunguza nafasi za kazi na mapato, kuongeza tisho la usalama, kusababisha maambukizo ya maradhi kama UKIMWI, uhamishaji wa watu; iwapo mradi utakuwa kwenye eneo linalokaribiana na misitu au hifadhi ya mbuga za wanyama pori na iwapo utaadhiri misitu na mimea kama mikoko. Kwa mfano ikiwa mradi unaohusika utahitilafiana na mhundo wa ardhi/nchi au kuwazuia watu wasifikie malisho kwa mifugo wao kwa urahisi, msimamo wa kufanya mabadiliko utabidi kuchukuliwa ili kuchukua mkondo mpya.

KULINDA MIMEA YA SHAMBANI

Maswala yanayoibuka hapa ni mengi, yakiwa ni pamoja na umuhimu wa kutumia madawa ya kuwauwa wadudu waharibifu, uchafuzi wa mazingira, hatari za madawa yenyewe, gharama na ulindaji wa mifugo.

Aina ya wadudu pamoja na mazingira yao muhimu pia zimeelezwa: kwa mfano wale wanaongilia mifugo, binadamu, maji na mimea. Njia tofauti za kukabiliana na wadudu hao katika mazingira yao zimetolewa na hatua za tahadhara pia kuelezwa. Watu wameelezwa pia jinsi ya kuhakikisha kuwa wamejilinda na kujikinga binafsi, wanyama wao, maisha yao na mimea yao ya shambani.

Hatari ya madawa ya kuwauwa na kukabiliana na wadudu ni kubwa. Hatua za tahadhara zinapasa kuchukuliwa wakati wa kutayarisha madawa hayo na pia yanapotumika. Kwa mfano Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema kwenye ripoti yake kwamba vifo vya watu 220,000 huripotiwa kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni kila mwaka. Tarakimu hizi hazitoi idadi ya watu wanaokufa nchini Kenya kutokana na hatari hii , lakini inatosha kuzingatia ukweli kwamba Kenya ni miongoni mwa mataifa ya ulimwengu na kwamba madawa mengi ya kuuwa wadudu waaribifu hutumiwa na watu kwa shughuli mbali mbali.

Kemikali hizi husambazwa na maji ya mvua (kutoka mashambani) na kuhatarisha maisha ya watumiaji maji, ikiwa na mifugo au wanyama wa porini, na hata wale viumbe wanaoishi kwenye maji.

Kuna ripoti kuhusu madawa hatari na yale yaliyopigwa marufuku na serikali. Mengi ya madawa haya hutumika kwa “kutibu” mchanga, kuuwa wadudu wanaoharibu matunda, mimea , nafaka na maboga. Jumla ya madawa kumi na saba (17) tofauti yameorodheshwa kwa manufaa ya watu. Kuna njia za kiasili zinazopendekezwa katika kukabiliana na wadudu waharibifu – kwa mfano utumiaji wa wadudu aina ya komba ambao wanaweza kuangamiza kwekwe kwenye maziwa. (Aina Fulani ya kwekwe hujitokeza kwenye maji na kutatiza samaki na shughuli za uvuvi kwa jumla. Maelezo yanatolewa kuhusu jinsi aina hii ya kwekwe (hyacinth) ilipomalizwa kwa njia hii katika maziwa ya Kyoga na Victoria katika miaka ya 1990).

Sehemu hii ya tatu pia ina michoro yenye vielelezo kuhusu matumizi salama ya madawa yanayohusika na yale yaliyopigwa marufuku au yale yasiyokubalika kwa utumiaji na watu bila usimamizi unaofaa.

- END -